BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Tatu – Tarehe 09 Septemba, 2022.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

74. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Ibara ya 133 na 134 za Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, zimeeleza bayana uwepo wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja ya kuwekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali zetu mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya pamoja ya Fedha kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, utekelezaji wa ibara hizi unaonekana kupuuzwa kwa muda mrefu.

(a) Kwa kuwa akaunti hii ilitakiwa kufunguliwa siku nyingi tu na hadi sasa haijafunguliwa, Je, ni lini akaunti hii ya pamoja itaanzishwa kwa maslahi ya pande mbili hizi za Muungano.

(b) Je, ni kiasi gani cha mapato hayo kimepatikana na kilitarajiwa kuhifadhiwa kwenye Akaunti ya Fedha ya pamoja.

### Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

2. MHESHIMIWA AZA JANUAR JOSEPH (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kumekuwa na utaratibu wa baadhi ya skuli za watu binafsi (Private Schools) kuwataka wanafunzi wao wanaopata daraja la nne (Division Four) katika muhula wa pili wa kidato cha tatu kuingia kidato cha nne, kurudia mwaka au kuchukuwa uhamisho na kwenda katika skuli nyengine.

(a) Je, kwa kiwango gani Wizara yako inalifahamu suala hili.

(b) Je, hawa wanafunzi wenye uwezo mdogo wa ufaulu wapelekwe wapi kusoma ikiwa kila skuli inataka wanafunzi wenye ufaulu wa juu pekee.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

84. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini): Namuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Napenda kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mabadiliko makubwa ya uendeshaji wa kiwanja cha ndege cha Zanzibar hasa katika maeneo ya kuondokea na kupokea abiria, sambamba na kuruhusu taasisi binafsi kuwekeza uwanjani hapo.

(a) Kwa kuwa moja ya maeneo muhimu ya viwanja vya ndege ni sehemu ya wageni mashuhuri (VIP) na kwa kuwa katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kulikuwa na wafanyakazi ambao hawajaajiriwa. Je, Serikali imechukua hatua gani za kuwaajiri wafanyakazi hao ili kuongeza ufanisi wa kazi katika eneo hilo muhimu.

(b) Katika viwanja vyote vya ndege duniani, Wageni Mashuhuri (VIP) huchukuliwa kwa gari yao maalum bila ya kuchanganywa na abiria wengine. Je, ni sababu zipi zinazopelekea abiria wa VIP Zanzibar kuchanganywa kwenye gari za abiria wa kawaida.

**Wizara ya Afya:**

51. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kitendo cha Mzazi kujifungua kinahitajika pahala penye utulivu sambamba na mzazi kupata huduma nzuri na yenye uweledi wa kutosha wa Mkunga (Intensively Nursing Care), jambo ambalo ni muhimu na lenye kuakisi afya ya mama na mtoto. Aidha, suala hilo ni adimu kupatikana kwenye vituo vingi vya afya kwani wakati mwingi wazazi hujifungua kwa kupata msaada wa mtumishi wa kawaida wa afya (Orderly) badala ya Mkunga mwenye uweledi.

(a) Je, hali ya mama mzazi kujifungua kwa msaada wa ‘Orderly’ inasababishwa na nini.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya tatizo la kukosekana kwa wakunga wenye uweledi na waliosomea kazi yao hii katika vituo vyetu vya Afya.

**<u>Wizara ya Biashara na Viwanda:</u>**

55. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kwakuwa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba bado kuna maeneo mbali mbali yaliyowazi na yaliyojitenga na maakazi ya watu. Na kwa kuwa maeneo hayo bado yako vizuri katika mambo ya uwekezaji katika sekta ya viwanda.

Je ni sababu gani za msingi tangu zamani na hadi sasa, zilizopelekea kiwanda cha kusindika mafuta ya Makonyo kilichopo Wawi kujengwa katikati ya maakazi ya watu.

**<u>Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

70. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kama inavyofahamika, ulimwengu unamtaka mwanamke kushiriki katika harakati mbali mbali zikiwemo za kisiasa kwa kupewa vipaumbele maalum. Hata hivyo, jamii imekuwa na wasiwasi juu ya maandalizi na matayarisho ya mtoto wa kike katika jamii zetu, kama kweli yanaweza kumfikisha kutimiza malengo aliyokusudiwa kuyatimiza.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kumuandaa mtoto wa kike ili kuyafikia malengo hayo.

(b) Je, ni yepi mafanikio ya miaka mitano iliyopita (2017-2022) katika kumuandaa mtoto wa kike ili kuyafikia malengo hayo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

37. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Kwa muda mrefu wakulima wa mpunga hutegemea mvua za msimu, hali ambayo imesababisha upatikanaji wa mpunga kupungua katika msimu mmoja hadi mwengine, kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi na hali ya hewa na kuwepo kwa jua kali. Ili kukabiliana na hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kutafuta mpango mbadala wa kukabiliana na

changamoto hiyo.

(a) Kwa kuwa Serikali ilianzisha mradi wa kilimo cha umwagiliaji maji na kukopa fedha kutoka “Exim Bank” ya Korea ya Kusini na kwa kuwa mradi huo ni muhimu kwa wakulima wa Zanzibar, Je, ni lini mradi huo unategemea kukamilika.

(b) Je ni kiasi gani cha fedha kitatumika hadi kumalizika kwa mradi huo.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

### Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Ripoti ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**09 Septemba, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**